## ALELUYA TUMWABUDU YESU KRISTU

Traditional
**Harmony by C. Saasita**




1. Sakramenti hii kuu ya mapendo,
   alipojiweka kwa ajili ye tu,
   nasi twakupa yetu leo mapendo.

2. Ni sadaka ya msalaba twaijua,
   kafufuka kisha kapaa kwa baba,
   yuko nasi katika hii Ekaristi.

3. Ni chakula chetu bora na kwa roho,
   ni mwanakondoo yule wa Paska,
   atulisha atushibisha daima.

4. Njoni wote tumwabudu Yesu Kristu
   nyoyo zetu nyimbo zetu tumtolee,
   sifa zetu shangwe zetu tumpatie.

5. Mwili wako uwe asili ya heri,
   utakase nyoyo zetu kwa damuyo,
   zifike mbinguni daima na milele.